# Fasihi ya Kiswahili na rushwa Tanzania: Thomas A. R. Kamugisha na *Kitu Kidogo Tu*

**E.S. Mwaifuge**
*Idara ya Fasihi, Chuo kikuu cha Dar es Salaam*

**I*kisiri***

Makala hii inajaribu kuelezea mchango wa fasihi ya Kiswahili katika kuijadili rushwa. Kwa kurejea kwenye Riwaya ya Thomas A.R. Kamugisha *Kitu Kidogo tu!* makala hii inasawilisha miongo takribani mitatu ya dhana ya "kitu kidogo" na athari zake kwa jamii ya Tanzania. Kwa kuijadili riwaya ya *Kitu Kidogo tu!* makala hii inajaribu pia kutoa picha ya Tanzania ya leo na kesho.

## 1.0 Utangulizi

Katika makala yake iitwayo "The lazy school of literary criticism" Armah (1985) akieleza mahusiano makubwa kati ya fasihi na binadamu anasema kuwa thamani ya kweli ya fasihi iko katika jambo la kimsingi la mahusiano na maingiliano ambayo inayawezesha baina ya jinsi tunavyoishi na jinsi tunavyofikiri – baina ya kuwako na tafakuri tunazokuwa nazo kuhusu kuwako huko.Katika maisha ya binadamu fasihi imekuwa kioo kinachotathmini maisha yetu ya kila siku katika nyanja zote za maisha.

Kwa kama miongo mitatu sasa fasihi ya Kiafrika imekuwa na ujumbe unaolezea madhara ya rushwa katika bara la Afrika. Waandishi wa ushairi, tamthiliya na riwaya wamekuwa wakieleza matatizo ya rushwa katika Afrika ya leo na pengine kutabiri Afrika ya kesho itakavyokuwa. Katika kujadili masuala ya rushwa waandishi wanatumia lugha za Kiafrika, na za kigeni hasa Kiingereza, Kireno na Kifaransa kama njia za kueleza athari za rushwa. Kazi hizi mbalimbali zinaelezea kiusanii chanzo cha rushwa kama umasikini, ubinafsi, utawala mbaya na kumomonyoka kwa maadili ya Kiafrika. Wito ambao umekuwa ukitolewa na waandishi ni kuwaasa Waafrika kukomesha rushwa ili kuimarisha utendaji wa Serikali zao na kuleta maendelelo ya kiuchumi na hatimaye kuboresha maisha ya watu wao.

Miongoni mwa waandishi wa Kitanzania walioijadili rushwa kiuyakinifu ni Thomas Kamugisha. Riwaya yake *Kitu Kidogot tu!* ni ya kihistoria inayoelezea historia ya rushwa Tanzania. Trotsky (1977) anabainisha kuwa riwaya ya kihistoria ni ile inayoakisi ukweli na inayoelezea uhalisi wa mazingira - yaani mahali yanapotokea matukio hayo, na muda au wakati wa matukio hayo yanayoelezwa. Luckacs (1962) anaongeza kuwa riwaya za kihistoria zinaunganisha matukio halisi yaliyopita, yaliyopo na pengine kutabili yajayo.

Riwaya ya Kitu Kidogo tu! inaakisi Tanzania ya 1984 na 1985. Katika kipindi hicho kulikuwa na hali ngumu ya uchumi iliyosababishwa kwa kiasi kikubwa na vita baina ya Tanzania na Uganda. Hali ngumu ya uchumi ilisababisha hali

ngumu kwa maisha ya watanzania. Kukosekana kwa bidhaa muhimu madukani, umasikini na udogo wa mishahara ya wafanyakazi ni hali ambazo zilisababisha dhana ambayo Kamugisha anaiita **kitu kidogo tu**, dhana ambayo leo imezaa rushwa kubwa. Katika kuyabainisha yote haya Kamugisha anaijenga historia ya Tanganyika na Tanzania kabla ya Uhuru, baada ya Uhuru hadi 1977 Chama cha Mapinduzi kilipozaliwa baada ya kuunganisha chama cha TANU na ASP.

Kwa kutumia hadithi na mashairi Kamugisha anavielezea vipindi hivi vitatu, kipindi cha kabla ya Uhuru, baada ya Uhuru (wakati wa TANU) na baada ya kuzaliwa CCM. Anaona kwamba TANU ilikuwa na maadili mema ya kitanzania yaliyoleta na kutetea haki, upendo na usawa miongoni mwa jamii ya watanzania. Pia anaona kwamba kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi ndiko kulikoleta wadhalimu, wadhulumaji, hali mbaya ya uchumi, umasikini na hatimaye rushwa (Uk. 52-54). Mwandishi anamtumia mwalimu Tadeo aliyeishi vipindi vyote vitatu kueleza:

> Mimi nilianza kazi ya ualimu mwaka 1951. Nimefundisha kwa miaka thelathini na ushahidi wa kazi yangu ni nyinyi hapa akina Musa… Nilifanya kazi chini ya serikali ya mkoloni, chini ya serikali ya TANU na chini ya serikali ya Chama cha Mapinduzi. Najua ubaya na uzuri wa serikali zote hizi isipokuwa ya Chama cha Mapinduzi hakika uzuri wake siujui… chini ya serikali ya mkoloni nilikuwa mwalimu hasa. Nilifanya kazi na kulipwa kila mwisho wa mwezi, nikienda likizo kwa gharama ya serikali. Chini ya Serikali ya TANU, vilevile sina la kulalamika lakini chini ya "Siri kali" ya Chama cha Mapinduzi… Yuko wapi mwalimu aliyekuwa nadhifu darasani na nje ya darasa? Aliyevaa viatu viilvyong'ara na stokingi nyeupe, kaptula nyeupe, shati nyeupe na tai kichwani? Yuko wapi yule mwalimu aliyekuwa mfano wa kuigwa, aliyeheshimiwa Kijijijni, mwalimu ambaye kila binti alitamani aolewe naye? Yuko wapi nauliza?… "Sirikali" ya CCM imemtoa wapi huyu? Yuko wapi mhaya? Yule nyirenju aliyevalia kanzu ya rasi na koti la zilungi, akaenda kwenye sosaiti akauza kahawa yake… (Uk. 57-58).

Mwandishi anatumia mfano wa maisha ya mwalimu wa Tanzania na wa kabila la Kihaya kama kiwakilisho cha matatizo ya Watanzania baada ya kuzaliwa CCM. Musa Nshomile, mhusika mkuu katika riwaya ya *Kitu Kidogo tu*! anarejea kutoka masomoni nchini Uingereza akiwa na ari kubwa ya kulitumikia taifa lake. Japokuwa anakatazwa na Irene (rafiki yake wa kike) kuwa asirudi Tanzania kwa sababu ya hali mbaya ya uchumi Musa yuko radhi kuikabili na kusaidia kuitatua hali hiyo. Anamwambia Irene:

> Lakini nitakaa hapa nifanye nini? Musa aliuliza. Nilikuja kusoma na tayari nimehitimu shahada zote zinazotolewa na vyuo vikuu vya hapa Uingereza katika fani yangu. Sana sana nimekaa zaidi ya ilivyotegemewa. Kazi sasa ni kwenda nyumbani kujiunga na wenzangu katika ujenzi wa taifa la Watnzania (Uk. 5).

Ndoto na matarajio ya Musa yanatoweka anapofika katika nchi yake. Aliondoka Tanzania wakati wa TANU na amerejea wakati wa CCM. Maisha mazuri na yenye matumaini yaliyokuwepo wakati wa TANU hayapo tena. Anayoyakuta Musa ni maisha mapya yaliyopoteza nuru na mwelekeo.

Dalili ya Tanzania mpya anayokuja kuikabili Musa zinajionyesha uwanja wa ndege wa kimataifa wa Dar es Salaam.Ili aweze kuruhusiwa kuingia nchini Musa anatakiwa atoe kitu kidogo (ahonge):

> "Bwana Nshomile unaweza kuchangia moja katika matatu."
>
> "Yapi hayo?"
>
> "Kwanza uko huru kabisa kurudi utokako."
>
> "Nitarudije Uingereza hali mimi ni Mtanzania? Tanzania ndiyo nchi pekee duniani ninayoijua kuwa ni yangu."
>
> "Basi kuna la pili. Unaweza kukaa hapa chini ya ulinzi wa polisi hadi hapo, afisa toka wizarani atakapokuja na dawa ya chanjo. Inaweza kuchukua siku na hata majuma kabla ya dawa kupatikana. Vinginevyo, na hilo ndilo la mwisho, unaweza kufanya kitu kidogo (uk.8).

Matukio ya kutakiwa kutoa kitu kidogo pale uwanja wa ndege ndiyo yanayoashiria maisha atakayombana nayo Musa Nshomile. Ili kupata huduma na mahitaji mbalimbali anayostahili Musa Nshomile anatakiwa atoe kitu kidogo – hongo. Mathalani, ili Musa aweze kupata nyumba ya serikali huduma ya usafiri, huduma za kiofisi na matibabu analazimishwa atoe kitu kidogo. Tangu mwanzo wa riwaya hii tunamuona Musa akikataa katakata kutoa rushwa kama anavyoeleza yeye mwenyewe kuwa hawezi kununua haki yake. Musa anamwambia afisa Uhamiaji wa uwanja wa ndege:

> "Kwa upande wangu siwezi," Musa alikataa. "Kwanza hizo dola sina, na hata ningekuwa nazo nisingekupa. Hiyo ingekuwa ni rushwa, na rushwa ni adui wa haki na huvunja heshima ya mtu" (Uk. 10).

Mwandishi anamchora Musa kama mtu mwenye msimamo, msomi na pengine mkombozi anayekuja toka masomoni nje ya nchi kuikomboa nchi yake iliyopoteza dira na mwelekeo. Tatizo linalomkabili Musa ni kwamba yuko peke yake. Hakuna anayemuunga mkono katika kuikataa rushwa. Jamii ya Tanzania inaonekana kuukubali "utamaduni" huu mpya. Ayittey (1999) na Geertz (2000) wanabainisha kwamba utumaduni ni muunganiko wa matukio yaliyopo kwenye jamii fulani ambayo humkuza mtu na kutawala tabia za makundi. Katika riwaya ya *Kitu Kidogo tu!* Kamugisha anajaribu kuelezea jinsi jamii ya Watanzania ilivyoikubali rushwa na kuifanya ni sehemu ya maisha:

> Baada ya abiria kuwaridhisha wale askari kwa "Kitu Kidogo" gari liliruhusiwa kuendelea na safari. Lakini halikwenda mbali ilipofika karibu na barabara iendayo kambi ya Jeshi ya Kaboya lilisimamishwa na polisi wa trafiki. Dereva na utingo wake walizungumza na hao wanausalama barabarani. Mara utingo alirudi kuwatangazia abiria, "Gari limekamatwa. Kama mnataka safari iendelee tuchangishe ushuru wa barabara." Bila kubishana kama ni kitu cha kawaida, abiria mmoja mmoja walianza kutoa shilingi mia (Uk. 48).

Mazingira yanaathiri maisha ya binadamu (Shorter 1998). Kama ilivyoelezwa hapo juu kuna mahusiano makubwa kati ya mazingira na tabia za binadamu. Mazingira yanaathiri tabia ya binadamu kwa kuwa mwanadamu hulazimika kufuata yale yanayomzunguka kama vile mitazamo ya maisha, mila, tamaduni, imani na maadili. Awali Musa Nshomile alikuwa mtu mwenye msimamo dhidi ya rushwa. Tunamwona anakataa kutoa rushwa kwa kuwa rushwa ni adui wa haki. Lakini Musa anaishi kwenye jamii iliyoikubali rushwa. Kwa kuwa hataki kutoa Kitu Kidogo maisha ya Musa yanaathirika kwa kila hali. Kidogo kidogo Musa anajikuta ameathirika na kuanza kushiriki kwenye rushwa, kwa kuwa kama binadamu anahitaji kuishi. Lakini pamoja na kushiriki katika rushwa Musa anateseka. Hana furaha kwani anajua anatenda maovu. Ubunifu wa Kamugisha katika riwaya hii ya *Kitu Kidogo tu!* unaonekana pale anapomjenga mhusika wake mkuu – Musa Nshomile katika hali ya kuteseka. Musa anajiona mpweke na mgeni katika nchi yake mwenyewe:

> Alikaa chini, akainamisha kichwa dhake. Kasi ya mapigo ya moyo wake ilikuwa ya kutisha. "Hapana" Musa alijisemea kwa sauti. "Hapa sitakiwi." Hapa mimi mpagani Kanisani. Wazo la jana yake, wazo la kuikimbia nchi yake lilimjia tena – Taswira ya maisha ya Ulaya ilikuwa mbele yake. Aliiona Manchester, alimwona Irene. Mara alifikia uamuzi. Angekwenda kuishi Ulaya(uk.112).

Kwa kumtumia Musa Nshomile mwandishi wa riwaya hii anajaribu kuiasa jamii ya Tanzania ibadili mienendo isiyokubalika. Kifasihi, mateso anayoyapata Musa yanatokana na matendo maovu yasiyokubalika katika jamii. Riwaya ya *Kitu Kidogo tu!* inaihamasisha jamii kufuata maadili mema. Katika makala yake iitwayo "Mwandishi wa Riwaya ya Kiswahili na suala la ukweli wa maisha" Madumula 1993:144) anasema:

> Katika majaribio ya awali ya uandishi wa riwaya za Kiswahili tunaweza kuona kuwa ijapokuwa mada inayahusu mazingira ya wakati wa sasa, na hivyo kuonyesha usasa wa wakati na mahali, msanii anatumia mbinu za zamani za kisanaa katika kuusawiri ukweli wa maisha; majaribo haya ya awali yanajitokeza katika mkondo wa riwaya ya Kimaadili – *Bildungserzaehlung* – ambayo lengo lake la msingi ni kufundisha maadili ya jamii. Namna msanii anavyofundisha maadili ya jamii tunapata katika jinsi alivyowachora wahusika wake ambao kwao anausawiri ukweli wa

> maisha. Na ni mhusika mkuu ndiye anayetumiwa kuufafanua, kuhubiri na kuutetea ukweli huo wa maisha. Mhusika huyu, kwa kiasi kikubwa, ana sifa za ki-tendi yaani ana nguvu za ajabu na ujasiri usio wa kawaida; ana sifa za uadilifu na akili zisizo na mpaka; tena ana hamu isiyolegea ya kutimiza lengo alilodhamiria kulitekeleza. Mhusika huyu amechorwa na msanii kwa makusudi mazima ya kuumba mfano bora wa kuigwa na kumfanya awe kielelezo cha ukweli na ukamilifu wa maisha…

Kwa kumtumia Musa, Kamugisha, ameweza kuelezea ukweli wa maisha ya Watanzania. Ameelezea rushwa ilivyokithiri katika sekta mbalimbali kama vile afya, elimu, ujenzi, usafiri na mahakama. Pamoja na hayo mwandishi amebainisha athari za rushwa. Mwalimu Tadeo, mwalimu Martin, mwalimu Mary, Abdu na Katoto ni miongoni mwa watu walioathiriwa na uwepo wa rushwa na kubadili kabisa mfumo wao wa maisha. Kwa mfano mwandishi anasawiri hali halisi ya "mfumo" wa mahakama na magereza nchini Tanzania:

> "Si rahisi kueleza", Abdu alisema. "Lakini nitajitahidi." Tulichukuliwa watu kumi na wawili kuisaidia polisi. Kama nilivyokwambia, hapo kituoni waliachiwa kina mama wawili. Kumi tulifikishwa mbele ya hakimu. Baada ya kesi kutajwa mara tatu, na ilikuwa ikitajwa kila baada ya wiki mbili, wenzetu watatu, akiwemo Mwenyekiti, walitoa Kitu Kidogo walifutiwa mashtaka, kwamba hapakuwepo ushahidi dhidi yao…. Watu walipoachiwa tulibaki saba. Baada ya Kesi kutajwa mara kumi hivi wenzetu wawili akiwemo balozi wangu Rwekaza, walitoroka katika mazingira ya kutatanisha. Tukabaki watano. Hapo ndipo viongozi walipoamua kutuhamishia katika Gereza lenye ulinzi mkali zaidi ya gereza hili. Hapo ndipo faili ya kesi yetu likapotea… Wenzangu walikufa… Wawili waliondolewa na kipindupindu wakati kilipolikumba gereza hili. Mmoja aliondolewa na Kiilemera*…." (Uk. 108-109).

Matumizi ya jina Kiilemera yanamrudisha msomaji nyuma kabisa ambapo eneo lenye jina hilo kule Mwanza ndiko ambako ambako mwaka 1968 watanzania 48 waliokamatwa kwa kushindwa kulipa kodi walifungwa kwenye kaselo kadogo na hatimaye kukosa hewa hadi kufa. Inawezekana kabisa kuwa ingekuwa enzi za Musa wa *Kitu Kidogo tu!* kitu kidogo kingetolewa hata kesi za watu hawa zingalifutwa.

Katika makala yake iliyotajwa hapo juu Madumulla (Uk. 146) anaongeza kuwa malengo ya waandishi wa kimaadili ni kugusia na kuzungumzia masuala mbalimbali yanayoigusa jamii na hata kuifundisha jamii juu ya maadili mema yanayotakiwa kufuatwa. Riwaya ya *Kitu Kidogo tu!* inakwenda mbali zaidi. Katika kuifundisha jamiii ya watanzania maadili mema – haki, utu, hekima, busara na matendo mema, Kamugisha anaijumuisha dini katika riwaya yake. Pengine, mwandishi anaona kwamba jamii ya watanzania imesahau miongozo ya dini na ndiyo maana inajishughulisha na matendo maovu. Wanataaluma kama

Pojman (1994), Magesa (1997) na Bujo (1998) wanaeleza kuwa maadili ndiyo asili ya dini kwa maana ya kwamba maadili yanahusianishwa na yanaelezwa kwenye imani za dini mbalimbali. Mojawapo ya kazi za dini ni kurekebisha na kuongoza maisha ya binadamu na pia kuelezea mambo mema na mabaya ili kujenga jamii iliyo bora na yenye mahusiano mema (Haviland, 1993). Kamugisha anaijumuisha dini kwenye riwaya ya *Kitu Kidogo tu!* kwa minajili ya kubadilisha tabia za watanzania. Mwalimu Tadeo anasali:

> …Ee Bwana Muumba vyote tunaomba ukiokoe kijiji chetu cha Mushule; uwaokoe watawaliwa na watawala wa kijiji hiki. Ee Bwana, ulituambia kupitia kinywa cha Mhubiri kwamba "Kisha nikarudi na kuona madhalimu yote yanayotendeka chini ya jua; na tazama, machozi yao waliodhulumiwa, ambao walikuwa hawana mfariji; na upande waliowadhulumu kulikuwa na uwezo walakini wale walikuwa hawana mfariji. "Kwa mantiki hii Ee Bwana tunakuomba uwafariji wote wanaodhulumiwa hapa kijijini na sehemu zote za nchi hii. Kwa mantiki hii hii ee Bwana tunakuomba uwafariji na wale wanaodhulumu kwani nao hawana mfariji. Uwafarijji wajumbe wa nyumba kumi wanaodai ujira bila ajira… uwafariji wenyeviti wa vijiji na wenyeviti wa vitongoji wanaonyang'anya mashamba ya wanakijiji na kufilisi maduka ya vijiji, uwafariji maafisa watendaji wa vijiji na maafisa watendaji wa Kata wanaotoza kodi ya maendeleo na kuifatuna wenyewe… Ee Bwana ulinena tena katika kinywa cha Mhubiri kwamba", Kweli jeuri humpumbaza mwenye hekima na rushwa uharibu ufahamu. Tazama Ee Bwana mahakimu wetu hawana tena ufahamu; sasa wanachukua rushwa toka kotekote, kwa mlalamikaji na mlalamikiwa na hivyo kukosa ufahamu wa kutoa hukumu ya watu wasio hatia kurundikana rumande… (Uk. 52).

Sala (maombi mbele ya mwenyezi Mungu) ni jambo kuu katika dini. Shorter (1998:77) anasema kuwa dini ni kiungo hai baina ya nuumini na Muumba wake; kwa hiyo ni jambo la masingi katika dini kwa kupoitia njia nyingi, zikiwemo sala, matambiko, mafunzo, na nyimbo. Sala inaonekana kuwa ni jambo linalouinua moyo na akili kujielekeza katika imani. Sala anayoitoa mwalimu Tadeo inalenga katika kumuomba mwenyezi Mungu aiokoe jamii ya Tanzania iliyozingirwa na udhalimu, dhuluma, uonevu na rushwa. Matendo haya yanahusianishwa na uovu - dhambi. Kupitia kwenye sala hii Kamugisha analenga kuzifundisha nafsi za Watanzania ziepukane na dhambi na kufuata maadili mema. Kama dini zinavyoeleza, dhambi inaharibu dunia iliyoumbwa na Mungu kwa mfumo maalum na pia inavunja mahusiano ya binadamu wenyewe na Mungu wao (Amaladoss, 1995).

Fasihi ina uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko, kwa kuwa inagusa hisia za binadamu. Riwaya ya *Kitu Kidogo tu!* imebeba ujumbe mzito kwa jamii ya Watanzania ambao leo hii wamo kwenye mapambano makubwa dhidi ya rushwa. Thomas Kamugisha ametuelezea historia ya rushwa Tanzania. Ijapokuwa masimulizi yake yanaishia mwaka 1985 (wakati wa awamu ya pili ya uongozi) Kamugisha hasiti kuimulika jamii ya Watanzania wa leo. Kama anavyosema

yeye mwenyewe Kamugisha, kitu kidogo cha miaka ya 1980 kimezaa rushwa kubwa ambayo imekuwa ngumu kuidhibiti.

Katika mahojiano na David Martin (Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti na Utunzaji Nyaraka cha Kusini mwa Afrika) Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa (1995:5) anakiri bayana kwamba tatizo kubwa linaloikabili Tanzania ni rushwa anaposema:

> …Corruption featured immensely. I raised the issue at all my meetings. There is a widespread feeling among the population as well as in the donor community, that it's a serious disease in our society, it is an impediment to justice and fairness, it has reached the point where it's a serious impediment to deveopment…

Maelezo hayo juu yanathibitisha kwamba rushwa ni "ugonjwa" mkubwa unaoikabili Tanzania. Kwa hiyo basi riwaya ya Kamugisha *Kitu Kidogo tu!* inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuielezea rushwa na maovu mengine ili kujaribu kuwabadilisha Watanzania wafuate mienendo bora na kujenga jamii yenye mahusiano mema.

## Marejeo

Amaladoss, M.S.J. 1995. *Creative Conflict: Theological Musings*. Bombay: St. Paul.

Armah, Ayi Kwei 1985. "The Lazy School of Literary Criticism." *West Africa* 3522:355-56.

Ayittey, George. B.N. 1999. *Africa in Chaos*. New York: St. Martin Griffin.

Bujo, Benezet. 1998. *African Christian Morality: At the Age of Inculturation*. Nairobi: Paulines Publications Africa

Greertz, Clifford. 2000. *The Interpretation of Cultures*. New York: Basic Books.

Haviland, W.A. 1993. *Cultural Anthropology*. New York: Harcourt Brace.

Kamugisha, Thomas A.R. 2000. *Kitu Kidogo tu!* Dar es Salaam: MPB Enterprises.

Luckacs, George. 1962. *The Historical Novel.* Penguin Books.

Madumulla, J.S. 1993. "Mwandishi wa Riwaya ya Kiswahili na Suala la Ukweli waMaisha" katika M.M. Mulokozi na C.G. Mung'ong'o, wah., *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji: Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania.* Uk. 141 – 153. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Magesa, Laurent. 1997. *African Religion: The Mmoral Traditions of Abundant Life.* Nairobi: Paulines Publications Africa.

Martin, David. 1995. *Buildilng a Vision: President Benjamin W. Mkapa of Tanzania:* Dar es Salaam: SARDC and African Publishing Group.

Ngugi wa Thiong'o 1996. *A Grain of Wheat.* London: Heinemann

_________________ 1977. *Petals of Blood.* New York: Penguin Books

_________________ 1982. *Devil on the Cross.* London. Heinemann Education Books.

Pojman, Lovis P. 1994. *Philosophy: The Pursuit of Wisdom.* Calfornia: Wadsworth Publishing Company.

Shorter, Aylward. 1998. *African Culture: An Overview, Social Cultural Anthropology.* Nairobi: Paulines Publications Africa.

Soyika, Wole. 1965. *The Interpreters.* London: Heinemann.

Trotsky, Leon. 1977. *On Literature and Art.* New York: Path Finder Press.